JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

| MAWASILIANO | |
|---|---|
| MKUU | 0754 630 967<br>0765 522 302 |
| M/MKUU | 0713 793 003 |
| MHASIBU | 0713 362 072 |
| PATRON | 0653 024 531 |
| **BARUA PEPE**<br>makogasecondary@gmail.com | |
| **ANWANI**<br>Mkuu Wa Shule,<br>Shule Ya Sekondari Makoga,<br>**S.L.P. 230, NJOMBE.** | |

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi: ______________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAKOGA HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2024/2025**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule ya **SEKONDARI MAKOGA** kwa mwaka wa masomo 2022-2023 kusoma tahasusi ya **HGK/CBG/HGFa**

1. MUHIMU SANA: SIMU HAZIRUHUSIWI SHULENI !!!!!!!!

2. MAHALI SHULE ILIPO:

Shule Ya Sekondari Makoga inapatikana mkoa wa NJOMBE Halmashauri Ya Wilaya Ya Wanging'ombe kata ya Makoga. Shule ipo umbali wa kilometa 31 Magharibi mwa mji wa Njombe.

Usafiri wa mabasi au magari madogo kama vile Noah na Probox unapatikana muda wote mchana kwa nauli ya shilingi 3000/- tu ukitokea kituo cha mabasi Njombe mjini **(NB: STENDI YA ZAMANI)** hadi kituo cha mabasi au stendi ya Makoga. Ufikapo stendi ya Makoga, panda pikipiki kwa nauli ya shilingi 1,000 tu hadi shuleni ambapo pana umbali wa kilomita moja pekee.

**Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe siku ya JUMANNE ya tarehe 01/07/2024** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia siku ya JUMATATU ya tarehe 01/07/2024. Siku ya mwisho kuripoti shuleni ni siku ya J**UMATATU** ya tarehe **08/07/2024.**

3. KAULI MBIU YA SHULE **"ELIMU NI UFUNGUO WA MAFANIKIO"**

Kauli mbiu hii ndiyo dira yako utakapokuwa hapa shuleni kwa kipindi chote cha miaka miwili ya masomo yako. Unatakiwa kuitafakari daima kwa vitendo. Hivyo, utatakiwa kuwa na tabia njema muda wote uwapo shuleni na uhudhurie masomo yote ukijifunza kwa bidii.

4. UJAZAJI WA FOMU:

Kabla ya kuripoti hakikisha unafanyiwa uchunguzi wa afya yako katika HOSPITALI YA WILAYA AU MKOA NA KUJAZIWA FOMU MAALUMU NA MGANGA MKUU. Fomu imeambatanishwa. Pia unatakiwa kujaza fomu ya kukubali kujiunga na shule ikiwa ni pamoja na kuandika mawasiliano sahihi ya mzazi au mlezi katika sehemu husika.

5. MICHANGO YA SHULE

Michango ambayo mwanafunzi anatakiwa kuilipia ipitie account namba ya shule **60601000015 NMB BANK** kwa jina la MAKOGA SECONDARY SCHOOL. Tafadhali, andika jina la mwanafunzi na mchepuo wake wa masomo (combination) kwenye **PAY IN SLIP**. Mwanafunzi ataiwasilisha kwa mhasibu mara afikapo shuleni.

a.) MICHANGO INAYOTAKIWA KULIPWA NA KILA MZAZI/ MLEZI

| NA. | AINA YA MCHANGO | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|
| i. | Uendeshaji wa shule kwa mwaka | 70,000/= |
| ii. | Tahadhari kwa mwaka (Haitarejeshwa) | 5,000/= |
| iii. | Kitambulisho cha mwanafunzi shuleni | 5,000/= |
| | **JUMLA YA MICHANGO** | **80, 000/=** |

- MICHANGO HII ITUMWE NMB BANK 60601000015 kabla ya kufika shuleni.
- **MUHIMU**: BIMA YA AFYA ndogo ya Tsh 6000/= ambayo inatumika zahanati na kituo cha afya tu au aje na bima kubwa itayompa nafasi ya kwenda kutibiwa hospitali kubwa. fedha ya bima ndogo **Fika nayo taslimu (CASH). Fedha hii ni kwa Yule asiye na kadi ya bima ya afya.**

b.) MAHITAJI MUHIMU KWA WANAFUNZI WOTE SHULENI

i. Mafaili mawili yakutunzia kumbukumbu muhimu shuleni.

ii. Ream moja ya karatasi ya A4 nyeupe. (kila mwaka). NA SIYO FEDHA.

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (Orodha imeambatanishwa).

iv. Dissecting kit kwa mwanafunzi wa masomo ya sayansi (BIOLOJIA).

v. Calculator kila mmoja (NB:Scientific Calculator fx 991watakaosoma sayansi)

vi. Godoro moja imara chapa Dodoma la futi 3 au kwa 6

vii. Vyombo vya chakula (KONTENA, KIKOMBE na KIJIKO).

viii. Mashuka mapya jozi mbili rangi ya bluu,

ix. Mto wa kulalia na foronya moja yenye rangi ya bluu

x. Blanketi kubwa nzito au ndogo mbili ni muhimu

xi. Tochi au Solata kwa ajili ya dharura wakati wa usiku.

## 6. SARE ZA SHULE:

### A. <u>SARE KWA WOTE:</u>

i. Sweta mbili za rangi ya kijivu

ii. Mashati meupe mawili (**MIKONO MIREFU).**

iii. Tai mbili rangi ya dark blue.

iv. T–shirt mbili rangi ya kijivu **ZIWE NA KOLA**

v. Koti jeupe mikono mirefu (laboratory coat) kwa watakaosoma sayansi tu.

vi. Track suit rangi ya kijivu isiyo na kofia (**SARE YA JIONI.)**

vii. Jezi za michezo t-shirt na bukta au suruali (**RANGI YA NJANO AU NYEKUNDU**.)

viii. Taulo na Ndala au kandambili za kuogea.

ix. Jaketi jeusi lisilo na kofia linaloishia **kiunoni, (LISIWE KOTI AINA YA SUTI).**

x. Toilet paper za kutosha (angalau 05)

xi. Sabuni za kutosha, mafuta ya kupaka na dawa ya mswaki

xii. Kiwi na brashi.

xiii. **Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba jozi mbili** (visigino vifupi) siyo bajaji.

xiv. **V**iatu vya michezo kama vile raba (**NB: SPORTS SHOES**).

xv. **PULLNECK NYEUPE mbili (02) ni muhimu sana**

## B. SARE NA MAHITAJI MUHIMU YA WASICHANA TU

i. Sketi 2 Dark-Blue Rindabox - istimu namba 01), (NB: **UREFU HADI KISIGINO**).

ii. Magauni 2 shamba dress rangi ya udongo, mshono solo, (Kitambaa ISTIMU NAMBA 01), mikono mifupi (**MUHIMU: urefu-hadi usawa wa kisigino).**

iii. Soksi ndefu nyeupe tu jozi au pair 02 (free-size) za kuvalia sare ya shule.

iv. Night dress mbili (02)

v. Kitenge (jozi au pair moja)

vi. Hijabu nyeupe za darasani (jozi 02) na nyeusi za jioni (jozi 02) zinazofunika mabega (**KWA WAISLAMU TU**).

vii. Nguo muhimu za ndani za kutosha.

## C. SARE NA MAHITAJI MUHIMU YA WAVULANA TU.

i. Suruali 2 dark blue, (ISTIMU NAMBA 01)

ii. Suruali 2 za rangi ya udongo Kitambaa ISTIMU NAMBA 01)

- Suruali ziwe na mifuko 03 (miwili mbele kulia na kushoto pembeni na mfuko mmoja upande wa nyuma mkono wa kulia)
- Suruali zote nne (04) ziwe na rinda mbili kila upande,
- **Suruali zote 04 ziwe na upana wa nchi 18 na mshono wa turn –up**.

iii. Nguo muhimu za ndani za kutosha.

iv. Soksi nyeusi tu jozi au pair 02 za kuvalia sare ya shule.

v. Mkanda wa suruali mweusi wa ngozi wa kawaida (**USIO NA UREMBO**).

### D. VIFAA VINGINE MUHIMU VINAVYOHITAJIKA SHULENI

i. Daftari kubwa kumi (10) aina ya kaunta

ii. Daftari ndogo (10) za mazoezi darasani.

iii. Mkebe mmoja, rula ndefu moja, Kalamu za wino (10) na kalamu za risasi (05).

iv. Ndoo kubwa moja ya lita 20 ya plastiki kwa ajili ya matumizi ya ofisi

v. Ndoo ndogo moja ya lita 10 (**NB: ndoo 02 za lita 10 kwa wanafunzi waislamu)**.

vi. Vitabu husika kulingana na orodha iliyoambatanishwa kwa kila somo

vii. Mvulana aje na **kwanja lililo nolewa lenye mpini wa mbao na squizer (mfagio wa kukaushia maji) moja** kwa ajili ya usafi.

viii. Msichana aje na **kwanja lililo nolewa lenye mpini wa mbao na soft broom (mfagio laini) moja** kwa ajili ya usafi.

## 7. MASHARTI MENGINEYO

**i. Mwanafunzi Afikapo Shuleni Awe Amevaa Track Suit Aliyoagizwa.**

ii. Mwanafunzi asije na nguo nyingine zaidi ya alizoagizwa, vinginevyo atarudishwa.

iii. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa mlinzi wa mwenzake katika kuzuia uovu unaoweza kutokea katika chumba chake cha kulala.

iv. Uharibifu wowote ule ukitokea katika chumba cha kulala kila mwanafunzi wa chumba husika ataadhibiwa sawa na wenzake

v. Uharibifu wowote ule ukitokea bwenini au darasani, kila mwanafunzi atalipa gharama husika kwani kila mmoja atakuwa amehusika katika uharibifu wa mali ya umma kama vile wizi, ajali ya moto au umeme n.k.

vi. Uharibifu utakaosababishwa na mwanafunzi ni jukumu lake na mzazi/mlezi wake.

## 8. MAWASILIANO TOKA KWA MZAZI:

i. Mawasiliano ya mzazi na mwanafunzi kwa muda ambao mwanafunzi atakuwa shuleni yatafanyika kwa namba za simu za shule **0758 81 40 25** (wavulana) na **0758 8138 56** (wasichana). Unaweza kutuma pesa za matumizi za mwanao kwa namba hizo pia na jina litasomeka **Makoga sekondari**

ii. Taarifa zote zinazomhusu mwanafunzi kama vile kufiwa zitumwe kwa mkuu wa shule na siyo mwanafunzi moja kwa moja. Vinginevyo haitasikilizwa.

iii. Mzazi/mlezi unaruhusiwa kumtembelea mwanao jumamosi ya mwisho ya mwezi tu.

## 9. USAFI BINAFSI:

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kuja shuleni akiwa na nywele fupi (usinyoe panki au upara).

ii. Hakuna ruhusa ya kufuga ndevu, kucha ndefu na kutumia vipodozi shuleni.

iii. Daima mwanafunzi anatakiwa kuwa nadhifu, msafi na aoge mara kwa mara.

## 10. UTUNZAJI WA AFYA NJEMA NA MAZINGIRA YA SHULE

i. Kila mwanafunzi atatakiwa kuyatunza mazingira ya shule katika hali ya ubora na usafi.

ii. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki kazi za mikono zenye lengo la kuendeleza elimu ya kujitegemea pamoja na kuimarisha afya ya mwili na mazingira ya shule.

## 11. SHERIA ZA SHULE NA KANUNI ZA SHULE

i. Mwanafunzi anatakiwa kusimama kumsalimia mtu yeyote anayemzidi umri wakati wote.

ii. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimiana na kushirikiana na wenzake.

iii. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kufanya kazi anazopewa.

iv. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu nembo zote za taifa kama vile bendera ya taifa.

v. Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi na kutunza mazingira ya shule vizuri.

vi. Mwanafunzi awapo shuleni lazima alale katika bweni na kitanda alichokabidhiwa pekee.

vii. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mfano mwema ndani na nje ya shule.

viii. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu ofisi zote za shule na majengo mengine yote.

ix. Mwanafunzi atahudhuria masomo kwa ratiba na kufanya mitihani yote inayomhusu.

x. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote shuleni kama vile; kupandisha bendera ya taifa, baraza la shule, mikutano ya bweni, darasa nk.

xi. Mwanafunzi anatakiwa kutii kengele kama mwito wa haraka.

xii. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare rasmi ya shule (**Darasani, Anapotoka nje ya shule, Anaporejea shuleni na Wakati wa baraza la shule).**

xiii. Mwanafunzi atatoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu ya;

- Mwalimu wa zamu na kuwepo tena shuleni kabla ya saa 12:00 jioni.
- Mkuu wa shule tu kwa kibali maalumu cha kulala nje ya shule.

**NB: Mwanafunzi akilala nje ya shule bila ruhusa atakuwa amejifukuza shule.**

xiv. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea nyumba za walimu na watumishi wengine ila kwa kibali maalum tu. Maeneo haya ni sawa na kuwa nje ya mipaka ya shule.

xv. Mwanafunzi haruhusiwi kuingiza mgeni yeyote bwenini au darasani bila idhini ya mkuu wa shule.

xvi. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea au kujihusisha na maeneo yafuatayo: Vilabu vya pombe (Bar) na Majumba ya kufikia wageni. (Guest houses).

xvii. Mwanafunzi anatakiwa kutunza mali zote binafsi pamoja na mali za umma kama vile madawati, vitanda, vifaa ya chakula, vitabu na vifaa vya maabara pamoja na majengo yote ya shule.

xviii. Mwanafunzi haruhusiwi kwa namna yoyote kumiliki au kutumia vifaa vinavyotumia umeme awapo shuleni kama vile:

- SIMU na RADIO
- Jiko La Umeme Au Heater,

- Vifaa vyote vya simu na radio kama vile: USB, CD, DVD, Earphones, Charger, Flash, Battery nk.

## 12. MAKOSA YANAYOPELEKEA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

- Wizi.
- Uasherati, ubakaji na ushoga.
- Uvutaji wa bangi na madawa ya kulevya.
- Kumtukana, kumpiga mwalimu au mtumishi wa shule.
- Kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- Kuoa, kuolewa, kusababisha utoaji wa mimba ndani nan je ya shule
- Kutoa lugha chafua au matusi.
- Kupatikana na makosa ya jinai.
- Kugoma, kuchochea au kuongoza migomo shuleni.
- Kukataa adhabu halali kwa makusudi.
- Kupatikana na simu au vifaa vya simu shuleni na nje ya mipaka ya shule.

## 13. NIDHAMU YA MWANAFUNZI

i. Ili uweze kujifunza na kufaulu masomo unatakiwa kuwa na nidhamu ya hali ya juu.

ii. Unatakiwa kuzisoma na kuzielewa vizuri sheria za shule zilizoambatanishwa na fomu hii.

iii. Fahamu kuwa si jukumu la shule kutoa nauli pindi mwanafunzi akipatikana na makosa ya kinidhamu yatakayomrudisha nyumbani. **NI JUKUMU LA MZAZI/MLEZI WAKE**.

## 14. DINI, MICHEZO NA UTAMADUNI

i. Kila mwanafunzi anaruhusiwa kufanya ibada kulingana na imani yake ili mradi shughuli za ibada zinaendeshwa kwa kuzingatia **SHERIA ZA NCHI NA RATIBA YA SHULE.** Aidha, mwanafunzi atafanya ibada ya sala au swala shuleni na katika nyumba za ibada katika maeneo yaliyo karibu na shule kwa ratiba na ruhusa maalumu.

ii. Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki michezo na utamaduni kwa lengo la kuleta uhusiano mwema na kujenga miili yenye afya. Hivyo, jitokeze na ibua kipaji chako katika fani mbalimbali kama vile kuimba, kuigiza, skauti na kadhalika.

## 15. CHAKULA MAALUMU

i. Shule **HAITATOA CHAKULA** maalumu kwa baadhi ya wanafunzi tofauti na wanafunzi wengine.

ii. Mwanafunzi haruhusiwi kuingia shuleni na chakula au kinywaji cha aina yoyote.

**<u>FOMU YA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI   MAKOGA</u>**

**A: MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI**

1. JINA LA MWANAFUNZI: ____________________________________________
2. TAREHE YA KUZALIWA: ___________________________________________
3. KIJIJI ALIPOZALIWA: ____________________WILAYA __________________
4. MKOA WA: ________________DINI:___________ DHEHEBU: _____________

**B: TAARIFA YA BABA NA MAMA MZAZI WA MWANAFUNZI**

1. JINA LA BABA: _____________________JINA LA MAMA: ________________
2. SIMU YA BABA: _____________          SIMU YA MAMA ________________
3. KAMILISHA TAARIFA ZA MAHALI ANAPOISHI MZAZI

   KIJIJI CHA: ______________   KATA YA: _______________

   WILAYA YA: ___________________   MKOA WA: __________ S. L. P. ______

**C: TAARIFA YA MLEZI WA MWANAFUNZI**

1. JINA LA MLEZI: __________________________________________________
2. NAMBA ZA SIMU: __________________________ AU ____________________
3. KAMILISHA TAARIFA ZA MAHALI ANAPOISHI MLEZI

KIJIJI: ______________ KATA:_______________WILAYA_________________

**D: TAARIFA YA AFISA MTENDAJI NA MWENYEKITI WA KIJIJI AU MTAA ANAPOISHI MZAZI/MLEZI**

1. JINA LA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI/MTAA:_____________________________
2. KIJIJI CHA /MTAA WA : ______________________ S.L.P. __________________
3. SIMU YA AFISA MTENDAJI: _______________________ AU _______________
4. JINA LA MWENYEKITI WA KIJIJI/MTAA:________________________________
5. KIJIJI CHA/MTAA WA: _________ S.L.P.________SIMU YA M/KITI:¬¬¬¬_________

MUHIMU: Ikiwa mzazi au mlezi wa mwanafunzi anahama kijiji au anabadilisha anwani au namba ya simu, taarifa itolewe shuleni mapema.

**Mimi mzazi au mlezi wa mwanafunzi______________________________ nakiri kuwa taarifa zilizojazwa hapo juu ni sahihi na kweli tu.**

SAHIHI YA MZAZI AU MLEZI: ______________________ TAREHE: _____________

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA - REQUEST OF MEDICAL EXAMINATION**

**MAKOGA SECONDARY SCHOOL**

P.O. BOX. 230,

NJOMBE.

PART A:

The Medical Officer,

……………………....District/Regional/Referral Hospital,

P.O. BOX…………………………………………….

……………………………………………………….

Please Examine Mr./Miss: ______________________________________ as to his or her physical and mental fitness for a full time schooling course. The examination should include the following categories (1-4) each category or sub category of which

will render the applicant's ineligibility in case of any defect.

1.
    a.) Eye – sight ………………………………………………………….…………………..
    b.) Hearing ……………………………………………………………………………
    c.) Limbs …………………………………………………………………………….
    d.) Speech …………………………………………………………………………….
    e.) Venereal diseases…………………………………………………………………….
    f.) Leprosy …………………………………………………………………….……….
    g.) Epilepsy ………………………………………………………………….……………….
2. Neuroses ………………………………………………………………………………
3. Other serious diseases …………………………………………….………………….
4. Pregnancy for girls ………………………………………………………..…………….

**Part B: MEDICAL CERTIFICATE (To Be Completed By A Medical Officer)**

I have examined the fitness of the above candidate and consider that he / she **is physically / mentally fit/unfit** for a full time schooling course for further studies.

Date of examination:_________________________ Signature:_________________________

**AHADI YA MWANAFUNZI**

**(IJAZWE NA KURUDISHWA KWA MKUU WA SHULE)**

1. Mimi__________________________________________________ nimesoma na kuelewa maelekezo, sheria, kanuni na taratibu za shule ya Sekondari Makoga. Nimekubali kuingia kidato cha _________ katika shule hii kuanzia tarehe ____________

2. Kwa hiyo, naahidi kwamba:

a.) Nitatii sheria zote za shule na kutimiza maagizo yote muhimu yaliyotajwa.

b.) Sitashiriki katika vitendo vya HUJUMA wala vitendo ambavyo vitakuwa ni kinyume na sheria zote za shule na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

c.) Nitatunza mali zote binafsi na shule kama majengo, samani, vitabu na kadhalika.

d.) Sahihi ya Mwanafunzi:________________________________________

e.) Tarehe ya kusaini fomu:________________________________________

**KIAPO AU AHADI YAMZAZI AU MLEZI WA MWANAFUNZI**

**Mimi__________________________________________ ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi____________________________________________________**

**NAAHIDI KWAMBA:**

1. Nitashirikiana kikamilifu na uongozi, walimu na wafanyakazi wote wa Shule ya Sekondari Makoga katika kumsaidia, kumlea na kumwelimisha mtoto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingatia sheria, taratibu na kanuni zote za shule na nchi ili aweze kutimiza maagizo yote yaliyotajwa hapo juu.

2. Nitafanya kila linalowezekana ili kumwezesha mwanangu kufika shuleni mapema. Nitamsaidia aweze kuishi mazingira mazuri ya kujifunzia. Nitamsaidia mahitaji yote muhimu ya shule kwa wakati wote akiwa shuleni.

3. Nitaitika wito wa mkuu wa shule na walimu ili niweze kusaidiana nao katika makuzi na malezi ya mwanangu ili afikie ndoto ya maisha yake kupitia Shule ya Sekondari Makoga.

**SAHIHIYA MZAZI / MLEZI: ____________________ TAREHE: ___________**

ORODHA YA BAADHI YA VITABU VYA A-LEVEL KWA KILA SOMO

A. VITABU VYA HISTORY

1. Modern World History (Ben Wash)
2. Africa In The World History (Nyirenda)
3. The Russian Revolution And The Bolshevic Victory (D.C. Heath & Company)
4. Major Events In The African History (Fr. Kamara).

B. VITABU VYA GEOGRAPHY

1. Certificate Physical And Human Geography (Goh Chang Leong).
2. A Comprehensive Approach To Physical Geography For Secondary School / Revised Ed.(D. T. Msabila : 2003)
3. An Integrated Regional Study On Human And Economic Geography Advanced Level Paper 2 : D. T. Msabila ;
4. Geography Ii Alive Human And Economic Geography. Kamili: Z.
5. Landforms In Africa (An Introduction To Geomorphology: C, Buckle (Longman: Malaysia)

C. VITABU VYA KISWAHILI

1. Kiswahili 1 Nadharia Ya Lugha , Kidato Cha Tano Na Sita Na Elimu Ya Juu. Suluhaya Masuku (2016) Stc Publisher. Dsm.
2. Nadharia Ya Lugha Kiswahili 1, Kidato Cha Tano Na Sita ( J. A. Masebo) 2016
3. Nadharia Ya Fasihi Kiswahili 2, Kidato Cha Tano Na Sita ( J. A. Masebo,
4. Sarufi Ya Kiswahili Sekondari Na Vyuo (Mdee, Dup-Dsm).
5. Kamusi Ya Kiswahili Sanifu – Tuki).

D. VITABU VYA CHEMISTRY

1. Dr. S. K. Jain (2018) Conceptual Chemistry For Class XI. S. Chand And Company Limited
2. Dr. S. K. Jain (2018) Conceptual Chemistry For Class XII. S. Chand And Company Limited
3. Advanced Chemistry Review ( William W. Davis; Mzumbe Bookshop Project, 2004.)
4. Physical Chemistry (Delungu Et Al: Mzumbe Bookshop Project, 1998).
5. Advanced Level Inorganic Chemistry Part I And Ii (Tanzania Institutue Of Education, 1995).
6. Organic Chemistry Vol. 1 The Fundamental Principles (I. L. Finar, Longman Ltd. 1990).

E. VITABU VYA BIOLOGY

1. New Understanding Biology (Susan Toole & Glenn 1999). Fourth Edition. Hutchinson Education. London UK
2. Biological Science; D. J. Taylor, N.P. O. Green & G. W. Stout. (2002) Third Edition, Cambridge University.
3. Advanced Biology Principles And Application (C.J. Clegg And D.G. Mackean.)
4. Advanced Biology (Michael Kent.)

F. VITABU VYA BASIC APPLIED MATHEMATICS

1. TIE (2016) Basic Applied Mathematics For Secondary Schools; Form V And VI
2. Sillem, S. (2013) Basic Applied Mathematics For Advanced Secondary Schools From V
3. Sillem. S. (2014) Basic Applied Mathematics For Advanced Secondary Schools For VI
4. Tie (2009) Basic Applied Mathematics For Secondary Schools, Form V And VI

## MUHIMU SANA KUKUMBUKA:

i. Fomu ya malipo ya michango ya mwanafunzi (**Pay slip original**)
ii. Cheti cha kuzaliwa na nakala yake **(original na copy)**
iii. Results slip (matokeo kidato cha nne) **(original na copy)**
iv. **Picha nne (04) za wazazi/ndugu wa karibu** wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

## UJAZAJI WA FOMU

**Kabla ya kufika shule ya sekondari Makoga jaza fomu zifuatazo kwa umakini.**

a.) Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi uliyopewa.

b.) Fomu ya kupima afya. (Medical examination form). Hakikisha fomu hii inajazwa katika hospitali ya serikali ya wilaya tu na si katika vituo vya afya.

c.) Kumbuka kuwa, unatoa taarifa sahihi juu ya hali ya afya yako ili shule iweze kukusaidia mara upatapo shida kwa haraka na si vinginevyo.

## MUHIMU SANA:

1. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni **kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi wa shule anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
2. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangia. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafuzi mmoja tu.

KUMBUKA: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yupo mahututi. Hivyo mzazi atume pesa.

Tafadhali, upatapo ujumbe kama huu usitume pesa yoyote, ni vema ukawasiliana na uongozi wa shule kupata ukweli wa taarifa husika kwa namba zifuatazo:

| MKUU WA SHULE | MAKAMU | MWL MWANDAMIZI MALEZI | MWL MWANDAMIZI TAALUMA |
|---|---|---|---|
| 0754 630 967 au 0765 522 302 | 0713 793 003 | 0653 024 531 | 0756 751 934 |

Tafadhali soma kwa makini maelezo na maagizo haya na kuyaelewa kwa ukamilifu.

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja SHULE YA SEKONDARI MAKOGA.

Nakala kwa:

- Katibu Ofisi ya Rais (TAMISEMI) S.L,P 1923 DODOMA
- Katibu Tawala Mkoa S.L.P. 668 NJOMBE
- Mkurugenzi Mtendaji Wanging'ombe S.L.P. 64 NJOMBE

**KARIBU SANA ______________**

**L. P. MULUNGU**

**MKUU WA SHULE**

**SARE ZA SHULE YA SEKONDARI MAKOGA**






